



JAMHURI YA MUUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



## TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA MASWALI YA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2022

MAARIFA YA JAMII



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



**TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI  
KATIKA MASWALI YA UPIMAJI WA KITAIFA WA  
DARASA LA NNE (SFNA) 2022**

**03 MAARIFA YA JAMII**

Kimechapishwa na;  
Baraza la Mitihani la Tanzania,  
S.L.P 2624,  
Dar es Salaam, Tanzania.

**©Baraza la Mitihani la Tanzania, 2023**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI .....	iv
1.0 UTANGULIZI .....	1
2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA KILA SWALI ....	2
2.1 Sehemu A: Maswali ya Kuchagua na Kuoanisha.....	2
2.1.1 Swali la 1: Kutambua Misingi ya Uzalendo Katika Jamii.....	3
2.1.2 Swali la 2: Kutambua Matukio Yanayotokea katika Mazingira Yanayomzunguka.....	13
2.2 Sehemu B: Maswali ya Majibu Mafupi .....	17
2.2.1 Swali la 3: Kufuata Kanuni za Kiuchumi Katika Shughuli za Uzalishaji Mali.....	18
2.2.2 Swali la 4: Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya kila Siku.....	27
3.0 TATHIMINI YA UFAULU KWA KILA UMAHIRI.....	31
4.0 HITIMISHO .....	31
5.0 MAPENDEKEZO .....	32
KIAMBATISHO .....	34

## **DIBAJI**

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa Taarifa ya Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi ya somo la Maarifa ya Jamii katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) 2022. Lengo la taarifa hii ni kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera, wakuza mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu kiwango cha ujifunzaji cha wanafunzi katika kipindi cha miaka minne ya Elimu ya Msingi.

Katika taarifa hii, mambo yaliyochangia ufaulu wa wanafunzi katika kila swali yameainishwa. Uchambuzi unaonesha kuwa, ufaulu mzuri wa wanafunzi katika maswali ulitokana na uelewa mzuri wa matakwa ya maswali na kuwa na umahiri wa kutosha katika somo. Pamoja na hayo, wanafunzi walikuwa na ufaulu hafifu walishindwa kutambua matakwa ya maswali kutokana na umahiri mdogo katika stadi za kusoma na kuandika na kutokuwa na umahiri katika maeneo yaliyopimwa.

Uchambuzi wa ufaulu wa wanafunzi katika kila umahiri ulifanyika na kuonesha kuwa, wanafunzi walikuwa mahiri katika; *Kutambua Matukio Yanayotokea Katika Mazingira Yanayomzunguka, Kutambua Misingi ya Uzalendo Katika Jamii, Kutumia Ramani na Elimu ya Anga Katika Maisha ya Kila Siku na Kufuata Kanuni za Kiuchumi Katika Shughuli za Uzalishaji Mali.*

Baraza la Mitihani la Tanzania linatarajia kuwa, mrejesho huu utaziwezesha mamlaka mbalimbaili za elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha michakato ya ufundishaji na ujifunzaji. Pia, Baraza linatarajia kuwa, changamoto zilizochangia ufaulu usioridhisha katika baadhi ya umahiri zitatatuliwa ili kuongeza ufaulu kwa wanafunzi wanaotarajiwa kuingia darasa la tano.

Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kutoa shukrani za dhati kwa wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii.



Dkt. Said A. Mohamed  
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) 2022 ulifanyika tarehe 26 na 27 Oktoba 2022. Jumla ya wanafunzi 1,718,896 walisajiliwa kufanya upimaji katika somo la Maarifa ya Jamii. Kati yao, wanafunzi 1,592,033 (92.62%) walifanya upimaji, ambapo, wanafunzi 1,354,141 sawa na asilimia 85.08 walifafulu.

Katika taarifa hii, utangulizi unafuatiwa na uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika kila swali. Uchambuzi unabainisha umahiri uliopimwa, ukiambatana na majibu ya wanafunzi ambayo yamegawanywa katika kiwango kizuri, cha wastani na hafifu. Sababu za kila kundi kuwa na umahiri walioonesha pia zimechambuliwa. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika kila swali umefuatiwa na tathimini ya ufaulu wa wanafunzi katika kila umahiri. Sehemu hiyo imefuatiwa na hitimisho pamoja na mapendekezo yaliyotokana na uchambuzi uliofanyika.

Viwango vya ufaulu wa wanafunzi vimezingatia asilimia ya wanafunzi waliofanya swali husika. Iwapo wanafunzi kati ya asilimia 0 hadi 33 tu ndio walioweza kujibu swali hilo vizuri, kiwango hiki cha ufaulu ni **hafifu**. Kwa upande mwengine, kama wanafunzi walioweza kujibu swali hilo vizuri ni kati ya asilimia 34 hadi 66, ufaulu huo ni wa **wastani**, na ikiwa wanafunzi walioweza kufanya swali hilo vizuri ni kati ya asilimia 67 hadi 100, kiwango hiki cha ufaulu ni **kizuri**. Katika uchambuzi huu, rangi ya kijani, njano na nyekundu zimetumika kuonesha ufaulu mzuri, wastani na hafifu mtawalia.

Karatasi ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne katika mwaka 2022 ya somo la Maarifa ya Jamii ilikuwa na maswali manne (04). Maswali hayo yaligawanywa katika sehemu kuu mbili; A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali mawili, swali la 1 na 2 yenye jumla ya

vipengele 14. Maswali hayo yalitoka katika umahiri mkuu wa *Kutambua Matukio Yanayotokea Katika Mazingira Yanayomzunguka na Kutambua Misingi ya Uzalendo Katika Jamii.*

Sehemu B pia ilikuwa na maswali mawili, la 3 na 4 yenyе jumla ya vipengele 11. Maswali hayo yalitoka katika umahiri mkuu wa *Kutumia Ramani na Elimu ya Anga Katika Maisha ya Kila Siku na Kufuata Kanuni za Kiuchumi Katika Shughuli za Uzalishajimali.* Wanafunzi walitakiwa kujibu maswali yote kutoka sehemu zote mbili.

## **2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA KILA SWALI**

Kwa ujumla, uchambuzi wa majibu ya wanafunzi ulionesha kuwa, kiwango cha ufaulu katika swali la 1 na 2 kilikuwa kizuri na cha wastani katika swali la 3, na hafifu katika swali la 4. Katika kuchambua kila swali vielelezo na chati vimetumika kuthibitisha hoja zilizotolewa.

### **2.1 Sehemu A: Maswali ya Kuchagua na Kuoanisha**


Sehemu hii iliundwa na maswali mawili yenyе jumla ya vipengele 14. Swali la 1 lilikuwa na vipengele nane (i)-(viii) vyę maswali ya kuchagua. Mwanafunzi alitakiwa kusoma swali na kisha kuchagua jibu sahihi kutoka katika machaguo aliyopewa na kuliandika katika kisanduku kilichoachwa wazi. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 16. Swali la pili lilikuwa na vipengele sita (i)-(vi) vyę kuoanisha. Mwanafunzi alitakiwa kusoma maswali kutoka fungu A, na kuoanisha na jibu sahihi kutoka fungu B.

### **2.1.1 Swali la 1: Kutambua Misingi ya Uzalendo Katika Jamii**

Jumla ya wanafunzi 1,592,033 (100%) walijibu swali hili, ambapo wanafunzi 12,603 (0.79%) walijibu kwa usahihi vipengele vyote nane na kupata alama 16, ambao ni ufaulu mzuri sana. Wanafunzi 218,780 (13.74%) walipata alama kuanzia 12 hadi 14 ambao ni ufaulu mzuri kwa kuwa waliweza kujibu kwa usahihi vipengele sita hadi saba vya swali hilo.

Kwa upande mwingine, jumla ya wanafunzi 92,2151 (57.92%) walipata alama kuanzia 6 hadi 10 ambao ni ufaulu wa wastani. Kati yao, wanafunzi 26,749 (16.80%) walijibu kwa usahihi vipengele vitano, wanafunzi 333,608 (20.95%) walijibu kwa usahihi vipengele vinne na wanafunzi 320,994 (20.16%) walijibu kwa usahihi vipengele vitatu.

Aidha, wanafunzi 438,499 (27.54%) walikuwa na ufaulu hafifu kwani walipata alama 0 hadi 4. Miongoni mwao, 60,347 (3.79%) hawakujibu kipengele chochote hivyo walipata 0. Wanafunzi 141,018 (12.63%) walijibu kwa usahihi kipengele kimoja na wengine 237,134 (14.89%) walijibu kwa usahihi vipengele viwili. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani wanafunzi 1,140,931 (72.46%) walipata alama kuanzia 6 hadi 16, kama inavyooneshwa kwenye Chati Na. 1.



**Chati Na 1:** Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 1

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika kila kipengele ulifanyika na kubaini mambo mbalimbali kama ifuatavyo:

- (i) Ni tukio gani la kihistoria lilitokea Tanganyika tarehe 9/12/1961?
- A Azimio la Arusha
  - B Muungano wa Tanganyika na Zanzibar
  - C Uhuru wa Tanganyika
  - D Tanganyika kuwa Jamuhuri

Katika kipengele hiki, mwanafunzi alitakiwa kubaini tukio la kihistoria lilitokea Tanganyika tarehe 09/12/1961. Kiwango cha ufaulu katika kipengele hiki kilikuwa kizuri kwani, wanafunzi wengi walichagua jibu sahihi C, *Uhuru wa Tanganyika*. Wanafunzi hao walikuwa na maarifa na ujuzi wa kutosha juu ya matukio ya kihistoria yaliyotokea katika nchi ya Tanganyika, hususani uhuru wa Tanganyika ambao ulipatikana tarehe 9/12/1961.

Pamoja na wanafunzi wengi kujibu kwa usahihi, baadhi yao walichagua kipotoshi *A*, *Azimio la Arusha*. Wanafunzi hao, walishindwa kutofautisha tukio la kupatikana kwa uhuru na tukio la kuzaliwa kwa Azimio la Arusha. Azimio la Arusha lilitangazwa rasmi na Mwalimu J. K. Nyerere tarehe 5/2/1967.

Zaidi ya hivyo, wanafunzi wengine walichagua kipotoshi *B*, *Muungano wa Tanganyika na Zanzibar*. Wanafunzi hao, hawakutambua kuwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulifanyika tarehe 26/4/1964 chini ya uongozi wa Rais Julius K. Nyerere na Aman Abeid Karume.

Vilevile, wapo wanafunzi waliochagua kipotoshi *D*, *Tanganyika kuwa Jamhuri*. Wanafunzi hao hawakuweza kutofautisha tukio la Tanganyika kupata uhuru na tukio la nchi hiyo kuwa Jamhuri. Kwa hiyo, wanafunzi waliochagua vipotoshi *A*, *B* na *D*, walidhihirisha kuwa na uelewa hafifu juu ya matukio ya kihistoria yaliotokea Tanganyika.

(ii) Zifuatazo ni faida za ngoma za asili **isipokuwa**

- A Kuendeleza utamaduni
- B Kupata hamasa ya kufanya kazi
- C Kupata zawadi mbalimbali
- D Kufanya mwili kuwa na afya

Swali lilimtaka mwanafunzi kubaini jambo ambalo siyo na faida ya ngoma za asili. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa mzuri kwani wanafunzi wengi waliweza kuchagua jibu sahihi *C*, *Kupata zawadi mbalimbali*. Wanafunzi hao waliweza kutambua faida za ngoma za asili kwa wapigaji pamoja na wachezaji. Jambo hili liliashiria kuwa, wanafunzi hao walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya kudumisha utamaduni wa Kitanzania.

Kwa upande mwingine, wapo wanafunzi waliochagua kipotoshi *A*, *Kuendeleza utamaduni*, *B*, *Kupata hamasa ya kufanya kazi na D*, *Kufanya mwili kuwa na afya*. Wanafunzi hao hawakutambua kuwa machaguo *A*, *B*, na *D* yanaelezea faida za ngoma za asili.

- (iii) Lughha, mipaka, utamaduni na Serikali kwa pamoja huunda
- A taifa.
  - B Jamhuri
  - C Bara
  - D raia.

Katika kipengele hicho, mwanafunzi alitakiwa kubaini kitu kinachoundwa na Lughha, mipaka, utamaduni na Serikali. Ufaulu wa wanafunzi katika kipengele hicho ulikuwa wa kiwango kizuri, kwani wanafunzi wengi walichagua jibu sahihi *A*, *taifa*. Wanafunzi hao walikuwa na uelewa kuhusu mambo yanayounda Taifa.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi walichagua kipotoshi *B*, *Jamhuri*. Wanafunzi hao, walishindwa kutofautisha dhana ya Jamhuri ambayo ni serikali inayoongozwa na Rais na huchaguliwa na wananchi na dhana ya taifa inayohusu mambo muhimu ambayo yanabainisha uwepo wa taifa fulani, yaani lugha, mipaka, utamaduni na serikali.

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi walichagua kipotoshi *C*, *bara*. Wanafunzi hao walikosa utambuzi wa ngazi mbalimbali za kimamlaka yaani nchi, bara na hatimaye Dunia. Bara ni sehemu kubwa ya nchi kavu ambayo imeundwa na nchi mbalimbali.

Vilevile, wapo wanafunzi waliochagua kipotoshi *D*, *raia*. Wanafunzi waliochagua kipotoshi hiki hawakuelewa kuwa, raia ni mtu anayeishi katika nchi fulani na kuwa na haki zote kama mzaliwa wa nchi yake.

Kwa mfano raia wa Tanzania, raia wa Kenya na raia wa Uganda. Hivyo, wanafunzi hao walichanganya dhana ya taifa na uraia. Kitendo cha wanafunzi kuchagua vipotoshi kiliashiria kuwa wanafunzi hao hawakuweza kutofautisha kati ya dhana ya taifa na dhana zilizowasilishwa na vipotoshi.

(iv) Yupi ni msimamizi mkuu wa shughuli za serikali katika Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania?

- A Spika
- B Rais
- C Waziri mkuu
- D Makamu wa Rais

Swali hili lilimtaka mwanafunzi kutambua kiongozi ambaye ni msimamizi mkuu wa shughuli za serikali katika Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa mzuri, kwani wanafunzi wengi walichagua jibu sahihi C, *Waziri Mkuu*. Wanafunzi hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu majukumu ya viongozi mbalimbali, hivyo kuwawezesha kutambua kuwa Waziri Mkuu ndiye msimamizi Mkuu wa shughuli za serikali Bungeni.

Vilevile, wapo wanafunzi waliochagua kipotoshi A, *Spika*. Wanafunzi hao walishindwa kutofautisha kati ya majukumu ya Spika na ya Waziri Mkuu. Wanafunzi hao walipaswa kuelewa kuwa kazi ya Spika ni kuratibu shughuli na majadiliano ya bunge. Spika huamua juu ya masuala ya utaratibu bungeni, mfuatano wa wabunge katika majadiliano na kutangaza matokeo ya kura bungeni. Yeye ndiye msimamizi wa taratibu za bunge kwa ujumla.

Wanafunzi wengine walichagua kipotoshi *B*, *Rais*. Wanafunzi hao, hawakuwa na uelewa kuhusu majukumu ya Rais na namna yanavyotofautiana na ya Waziri Mkuu kuhusu shughuli za Bunge. Wanafunzi hao, walipaswa kuelewa kuwa Rais ndiye Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali na Amirijeshi Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua kipotoshi *D*, *Makamu wa Rais*, walishindwa kuelewa kuwa Makamu wa Rais ndiye msaidizi na mshauri mkuu wa Rais kuhusu mambo yote ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, humsaidia Rais katika kufuatilia utekelezaji wa kila siku wa mambo ya muungano. Pia, hufanya kazi zote anazoagizwa, na Rais na hufanya kazi zote za Rais kama Rais hayupo kazini au akiwa nje ya nchi.

- (v) Yupi kati ya marais wa Tanzania alihusika katika kuanzishwa kwa Muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar?
- A Dkt. Jakaya M. Kikwete
  - B Benjamin W. Mkapa
  - C Samia Suluhu Hassan
  - D Julius K. Nyerere

Swali lilimtaka mwanafunzi kubaini Rais wa Tanzania aliyeusika katika kuanzishwa kwa Muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa mzuri kwani wanafunzi wengi walichagua jibu sahihi *D*, *Julius K. Nyerere*. Uchaguzi wa jibu hilo uliashiria kuwa wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu waasisi wa Muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar. Walitambua kuwa, Rais Julius K. Nyerere ndiye aliyeasisi Muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar tarehe 26/4/1964, akishirikiana na

Rais Shekh Abeid Aman Karume wa Zanzibar. Hivyo, wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya kuthamini mashujaa wetu.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi walichagua kipotoshi *A*, *Dkt. Jakaya M. Kikwete*. Wanafunzi hao walishindwa kutambua mtiririko wa matukio ukihusisha marais waliokuwa madarakani. Wanafunzi hao hawakubaini kuwa Dkt. Jakaya M. Kikwete alitawala Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 2005 hadi 2015 wakati muungano ulikuwa mwaka 1964. Wanafunzi wengine walichagua kipotoshi *B*, *Benjamin W. Mkapa*. Wanafunzi hao walishindwa kuelewa kuwa Rais Benjamin W. Mkapa alitawala Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 1995 hadi 2005. Hivyo, hiyo ni miaka 31 baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Vilevile, wanafunzi wengine waliochagua kipotoshi *C*, *Samia Suluhu Hassan*. Wanafunzi hao, hawakuwa na uelewa wa marais waliopita na Rais aliyeo madarakani. Kwa ujumla, wanafunzi hao walikosa maarifa kuhusu matukio mbalimbali nchini Tanzania, na rais aliyehusika na tukio husika.

(vi) Kundu lipi hujumuisha familia ya watoto yatima?

- A Mama na Watoto
- B Watoto bila wazazi
- C Watoto bila ndugu
- D Watoto wa mitaani

Swali hili lilimtaka mwanafunzi kubaini kundi linalowakilisha dhana ya familia ya watoto yatima. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani wanafunzi wengi walichagua jibu sahihi *B Watoto bila wazazi*. Wanafunzi hao walibaini kuwa familia ya watoto yatima inahusisha watoto ambao wazazi wao wote wamefariki.

Wanafunzi waliochagua kipotoshi *B*, *Familia ya mzazi mmoja*, hawakuwa na dhana sahihi ya uyatima. Familia ya mzazi mmoja haiendani na dhana ya yatima kwani watoto hupata malezi ya mzazi aliyepo.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua kipotoshi *C*, *Watoto bila ndugu*, hawakuwa na uelewa wa dhana ya familia kwa kuwa hii siyo aina ya familia. Wanafunzi hao walipaswa kuelewa kuwa watoto bila ndugu ni watoto ambao wazazi wao, wala ndugu zao hawajulikani. Kwa mfano, watoto wachanga waliotelekezwa au kutupwa.

Vile vile, wanafunzi wengine walichagua kipotoshi *D*, *Watoto wa mitaani*. Wanafunzi hao hawakuweza kupambanua kati ya dhana ya watoto yatima na watoto wa mitaani. Watoto wa mitaani huzurura mitaani ili kujipatia mahitaji yao. Watoto hao wanaweza kuwa yatima, watoto waliotelekezwa na wazazi na ndugu zao, au waliotoroka au waliokimbia kwao kwa sababu mbalimbali kama vile umaskini, ukatili wa baadhi ya wazazi au ndugu.

(vii) Zifuatazo ni aina za ukabaila zilizokuwepo Tanzania,  
**isipokuwa**

- A Umwinyi
- B Ubugabire
- C Nyarubanja
- D Ujamaa

Swali lilimtaka mwanafunzi kubaini mfumo ambao haukuwa wa ukabaila nchini Tanzania. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa ni wa kiwango cha wastani kwani, baadhi ya wanafunzi walichagua jibu sahihi *D*, *Ujamaa*. Wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mifumo mbalimbali ya kiuchumi nchini

Tanzania. Pia, waliweza kutambua sifa za mfumo wa kikabaila na ujamaa. Hivyo, walitambua kuwa, ujamaa ni mfumo wa uzalishaji mali ambao vitu vyote humilikiwa na wanajamii wote au serikali kwa niaba ya wanajamii. Hii inadhihirisha kuwa, wanafunzi hao walikuwa na ujuzi na uelewa mzuri kuhusu ukabaila na aina zake, hususani shughuli za uzalishaji mali katika jamii.

Kinyume na hapo, wanafunzi wengine walichagua Kipotoshi A, *Umwinyi*, B, *Ubugabire* na C, *Nyarubanja*. Wanafunzi hao hawakutambua kuwa mifumo hiyo iliwalishaa aina za ukabaila nchini Tanzania. Umwinyi ulikuwa ni aina ya ukabaila uliokuwepo maeneo ya Pwani ya Afrika ya Mashariki. Mfumo huu wa uchumi na utawala ulioongozwa na Mwinyi na ardhi ndiyo ilikuwa msingi mkuu wa uzalishaji mali. Kipotoshi B, *Ubugabire* ni mfumo wa uzalishaji mali uliojikita katika umiliki wa mifugo Magharibi mwa Tanzania, hususani Kigoma na nchi jirani za Rwanda na Burundi. Vile vile, C, *Nyarubanja* ni mfumo wa ukabaila uliojikita katika umiliki wa ardhi uliotumiwa na jamii za kale huko Karagwe.

(viii) Mfumo upi wa uzalishaji mali ambao jamii zote zimepitia?

- A    Ubepari
- B    Ujamaa
- C    Ujima
- D    Ukabaila

Swali hili lilimtaka mwanafunzi kubaini mfumo wa maisha wa uzalishaji mali ambao jamii zote zilipitia. Ufaulu katika swali hili ulikuwa ni mzuri kwani wanafunzi wengi walichagua jibu sahihi C, *Ujima*. Wanafunzi hao walikua na maarifa na ujuzi wa kutosha kuhusu mifumo ya kiuchumi na utawala. Hii ilisababisha kuwa rahisi

kwa wanafunzi hao kubaini kuwa kila jamii hapa duniani ilipitia katika mfumo huu.

Aidha, wanafunzi wengine walivutwa na kipotoshi A, *Ubepari*. Wanafunzi hao hawakuweza kuchambua mtiririko wa mifumo ya uzalishaji mali ilivyojitokeza. Hawakutambua kuwa, ubepari ni mfumo wa uchumi ambamo biashara, viwanda na vitegauchumi vingine vinatawaliwa na watu binafsi kwa kiasi kikubwa na kwa lengo la kupata faida. Nafasi ya serikali ni ndogo. Vilevile, lengo la kuhudumia jamii katika mahitaji yake haliongozi mipango.

Aidha, wanafunzi wachache walivutiwa na kipotoshi C, *Ujamaa*, kwa sababu ya kufanana kwa baadhi ya sifa za mfumo wa ujamaa na ujima. Katika ujima, njia kuu za uzalishaji mali zilimiliwi na jamii nzima na uzalishaji ulifanyika kwa pamoja, na vivyo hivyo katika mfumo wa ujamaa. Kwa ujumla, wanafunzi hao walipaswa kuelewa kuwa ujamaa haukuwa mfumo wa mwanzo wa uzalishaji mali. Kipotoshi hiki pengine kilivutia wanafunzi hao kwa sababu ya umaarufu wa siasa ya Ujamaa na Kujitegemea wakati wa Azimio la Arusha miaka ya 1967-1985.

Vilevile, wanafunzi waliochagua kipotoshi D, *Ukabaila* walishindwa kubaini ni mfumo upi kati ya ukabaila na ujima ulipitiwa na jamii zote. Ukabaila ni mfumo wa uchumi na utawala ambao ardhi ilikuwa msingi mkuu wa uzalishaji mali. Katika mfumo huu, ardhi ilimiliwi na watu wachache waliojulikana kama mabwana. Mabwana waliwafanyisha watwana (watu wasiokuwa na ardhi) kazi. Hata hivyo, siyo jamii zote zimepitia mfumo huo.

## **2.1.2 Swali la 2: Kutambua Matukio Yanayotokea katika Mazingira Yanayomzunguka**


Katika swali hili, wanafunzi walitakiwa kuoanisha Fungu A na B, na kisha kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano waliyopewa. Swali lilikuwa kama ifuatavyo:

Jibu kipengele cha (i-vi) kwa kuoanisha matumizi ya kifaa kinachotumika kufanya usafi maeneo ya shule katika **Fungu A** na aina ya kifaa husika katika **Fungu B**. Andika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano uliopewa.

<b>Fungu A</b>	<b>Herufi</b>	<b>Fungu B</b>
(i) Kukata miti mikubwa na matawi.	( )	A. Dekio
(ii) Kupunguza matawi ya miti.	( )	B. Shoka
(iii) Kupalilia.	( )	C. Fyekeo
(iv) Kukusanya takataka.	( )	D. Jembe
(v) Kubeba takataka.	( )	E. Toroli
(vi) Kuondoa tandabui.	( )	F. Fagio G. Panga H. Reki

Swali hilo lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kutambua Matukio Yanayotokea katika Mazingira Yanayomzunguka* katika umahiri mahsus wa *Kutunza Mazingira ya Jamii Inayomzunguka*. Swali lilipima umahiri wa wanafunzi katika kubaini vifaa vya usafi, na namna vinavyotumika katika kufanya usafi wa mazingira ya shule. Swali hilo lilikuwa na jumla ya alama 12.

Swali hili lilijibwa na wanafunzi 1,592,033 (100%). Kati yao, wanafunzi 165,251 (10.38%) walipata alama zote 12 ambao ni ufaulu mzuri sana, na wanafunzi 507,726 (31.89%) walipata alama kuanzia 8 hadi 10 ambao ni ufaulu mzuri. Kwa upande mwingine, wanafunzi 510,523 (32.07%) walipata alama 4 hadi 6 ambao ni ufaulu wa wastani, na wanafunzi 408,533 (25.66%) walipata alama 0 hadi 2 ambao ni ufaulu hafifu. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa sababu wanafunzi 1,183,500 (74.34%) walipata alama kuanzi 4 hadi 12 kama inavyoonekana katika Chati Na. 2.



**Chati Na 2:** Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 2

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi ulionesha kuwa, wanafunzi 165,251 (10.38%) waliojibu vipengele vyote sita kwa usahihi, na kupata alama zote 12, walikuwa na umahiri wa kutosha katika umahiri mahsusini wa *Kutunza Mazingira ya Jamii Inayomzunguka*. Wanafunzi hao walioanisha vifaa vinavyotumika katika kufanya usafi katika maeneo ya shule, na aina ya vifaa hivyo. Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali hilo.

2. Jibu kipengele cha (i) – (vi) kwa kuoanisha matumizi ya kifaa kinachotumika kufanya usafi maeneo ya shule katika **Fungu A** na aina ya kifaa husika katika **Fungu B**. Andika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano uliyopewa.

<b>Fungu A</b>	<b>Herufi</b>	<b>Fungu B</b>
(i) Kukata miti mikubwa na matawi.	( B )	A. Dekio
(ii) Kupunguza matawi ya miti.	( G )	B. Shoka
(iii) Kupalilia.	( D )	C. Fyekeo
(iv) Kukusanya takataka.	( H )	D. Jembe
(v) Kubeba takataka.	( E )	E. Toroli
(vi) Kuondoa tandabui.	( F )	F. Fagio
		G. Panga
		H. Reki

**Kielelezo Na. 2.1:** Sampuli ya majibu ya wanafunzi aliyejibu kwa usahihi vipengele vyote sita vya swali la 2

Kwa upande mwingine, wanafunzi 507,726 (31.89%) walioanisha kwa usahihi vipengele vinne hadi vitano, hivyo walipata alama 8 hadi 10. Wanafunzi hao walielewa vizuri baadhi ya vifaa vya usafi na matumizi yake, hivyo, kuoanisha kwa usahihi vipengele (i), (ii), (iii), na (iv) vya fungu A, kwa herufi B, G, D na H. Hata hivyo, hawakuoanisha kwa usahihi kipengele kimoja au viwili.

Aidha, wanafunzi wengi hawakuoanisha kwa usahhihi vipengele (v) na (vi) kwa herufi E *Toroli* na F *Fagio* mtawalia na kufanya wasipate alama zote. Hii ni kutokana na vifaa hivyo kuwa na matumizi zaidi ya moja katika kufanya usafi katika mazingira. Kwa mfano, fagio hutumika pia katika kufagilia na toroli hutumika pia kubeba mizigo mbalimbali kama vile magogo ya miti na matawi.

Uchambuzi zaidi wa majibu unaonesha kuwa, wanafunzi 510,523 (32.07%) walifaalu kwa kiwango cha wastani kwa kupata kati ya alama 4 hadi 6 kwa sababu walikuwa na uelewa wa wastani juu ya

ya vifaa vya usafi na matumizi yake. Wanafunzi wengi katika kundi hili walipata alama 6 kwani walioanisha kwa usahihi vipengele 3 kati ya 6 walivyopewa kwenye swalii. Wengi wa wanafunzi hao walioanisha kwa usahihi vipengele (ii), (iii) na (iv).

Wanafunzi waliojibu kwa usahihi kipengele cha (ii) walieleza kifaa kinachotumika kupunguza matawi ya miti kuwa ni Panga. Wanafunzi waliooanisha kipengele cha (iii) kwa usahihi walifahamu kuwa kifaa kinachotumika kupalilia, kulima na kuchimba mashimo kuwa ni jembe. Vilevile, wanafunzi waliooanisha kwa usahihi kipengele cha (iv) walikuwa na ujuzi wa matumizi ya reki katika kukusanya takataka kama vile nyasi na majani yanayodondoka kutoka mitini.

Hata hivyo, wanafunzi wengi hawakujibu kwa usahihi vipengele (i), (v) na (vi). Kwa mfano, hawakutambua kuwa pamoja na shoka kutumika kuchanja kuni, hutumika pia kukata miti mikubwa na matawi. Aidha, pamoja na toroli kutumika kubeba mizigo, hutumika pia kukusanya takataka. Fagio pia hutumika kuondoa tandabui pamoja na kufagilia mazingira.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, wanafunzi 408,533 (25.66%) walikuwa na ufaulu hafifu. Kati yao, wanafunzi 197,495 (12.41%) walipata 0 kwa sababu hawakuoanisha kwa usahihi vifaa vya usafi na matumizi yake. Wanafunzi 211,038 (13.26%) waliobaki walipata alama 2 kwani walioanisha kwa usahihi kipengele kimoja tu. Kipengele cha (iii) ndicho kilijibowi kwa usahihi na wanafunzi wengi zaidi wa kundi hili. Wanafunzi hao walikuwa na uelewa mzuri juu ya matumizi ya jembe, ambayo ni kupalilia, kulima na kuchimba mashimo. Hii inaonesha kuwa wanafunzi hao walikuwa na ufahamu wa kutosha ya matumizi ya jembe katika mazingira yaliyowazunguka.

Aidha, wanafunzi waliopata 0 hawakuwa na umahiri kuhusu vifaa vya usafi na matumizi yake. Wanafunzi hao walishindwa kuoanisha kwa usahihi vifaa na matumizi yake katika kufanya usafi wa mazingira ya shule. Hii ilidhihirisha kuwa wanafunzi hao hawakuelewa matakwa ya swali, au hawakuwa na maarifa ya kutofautisha matumizi ya vifaa husika. Kielelezo Na. 2.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi ambaye alishindwa kujibu kwa usahihi vipengele vyote vya swali la 2.

2. Jibu kipengele cha (i) – (vi) kwa kuoanisha matumizi ya kifaa kinachotumika kufanya usafi maeneo ya shule katika **Fungu A** na aina ya kifaa husika katika **Fungu B**. Andika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano uliyopewa.

<b>Fungu A</b>	<b>Herufi</b>	<b>Fungu B</b>
(i) Kukata miti mikubwa na matawi.	( D )	A. Dekio
(ii) Kupunguza matawi ya miti.	( A )	B. Shoka
(iii) Kupalilia.	( B )	C. Fyekeo
(iv) Kukusanya takataka.	( D )	D. Jembe
(v) Kubeba takataka.	( B )	E. Toroli
(vi) Kuondoa tandabui.	( D )	F. Fagio
		G. Panga
		H. Reki

**Kielelezo Na. 2.2:** Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi vipengele vyote vya swali la 2

## 2.2 Sehemu B: Maswali ya Majibu Mafupi

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili ya majibu mafupi, swali la 3 na 4. Katika swali la 3, wanafunzi walitakiwa kusoma kifungu cha habari na kisha kujibu maswali yanayotokana na kifungu hicho. Swali hilo ilikuwa na jumla ya vipengele saba vyenye alama 2 kila kimoja, hivyo kufanya jumla ya alama kuwa 14. Katika swali la 4,

wanafunzi walitakiwa kubainisha vipengele vinne muhimu vyatuzingatia wakati wa uchoraji wa ramani. Kila kipengele kilikuwa na alama 2, hivyo kufanya swali kuwa na jumla ya alama 8. Uchambuzi wa majibu unaonesha kuwa, ufaulu katika swali la 3 ulikuwa wastani na wa hafifu katika swali la 4.

### **2.2.1 Swali la 3: Kufuata Kanuni za Kiuchumi katika Shughuli za Uzalishaji Mali**

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kufuata Kanuni za Kiuchumi Katika Shughuli za Uzalishaji Mali* na umahiri mahususi wa *Kuthamini na Kulinda Rasilimali za Nchi*. Katika swali hilo, wanafunzi walitakiwa kusoma habari kuhusu Maliasili katika Wilaya yetu, kisha kujibu vipengele vilivyoulizwa kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi.

Swali hilo lilikuwa na vipengele saba, yaani (i) hadi (vii). Kipengele cha (i) kilipima ufahamu wa wanafunzi kubaini faida za rasilimali katika jamii. Kipengele cha (ii) kilimtaka mwanafunzi kutaja faida moja ya uvuvi. Kipengele cha (iii) kilipima uwezo wa mwanafunzi kubaini aina ya samaki anaevuliwa mtoni, na kipengele cha (iv) kilimtaka mwanafunzi kubaini aina ya uvuvi unaofanyika baharini. Aidha, kipengele cha (v) kilimtaka mwanafunzi kubaini athari zinazosababishwa na uvuvi wa samaki wachanga. Kipengele cha (vi) kilimtaka mwanafunzi kubaini njia inayotupatia samaki wengi. Mwisho, kipengele cha (vii) kilipima ufahamu wa mwanafunzi kutambua athari ya kuvua samaki kwa kutumia wavu wenye matundu madogo. Swali hilo lilikuwa na jumla ya alama 14. Kielelezo Na 3.1 kinaonesha habari iliyyotumika katika swali la 3.


3. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi ilioachwa wazi.

Wilaya yetu ina utajiri mwingu unaotokana na maliasili tulizonazo. Maliasili hizi huwezesha kufanyika kwa shughuli nyingi za kiuchumi ambazo huingizia wilaya yetu fedha nyingi. Tuna mto na bahari ambapo samaki huvuliwa kwa ajili ya chakula na biashara.

Uvuvi wa kwenye mto huitwa uvuvi wa maji baridi na samaki wake huitwa samaki wa maji baridi. Uvuvi unaofanyika baharini huitwa uvuvi wa maji chumvi na samaki wake huitwa samaki wa maji chumvi. Uvuvi huwapatia wakazi ajira na fedha. Njia mbalimbali hutumika katika uvuvi kutegemea eneo na aina ya samaki. Kuna uvuvi wa kutumia nyavu au ndoano. Wavuvi wanaotumia wavu hupata samaki wengi zaidi kuliko wale wanaotumia ndoano. Wavu ukiwa na matundu madogo huwa na athari kwani huvua samaki wakubwa na wachanga. Samaki wachanga wakivuliwa eneo hilo litakosa samaki siku za baadae.

***Kielelezo Na. 3.1: Kifungu cha habari ambacho wanafunzi walitakiwa kusoma na kisha kujibu swali la 3***

Uchambuzi unaonesha kuwa, swali hili lilijibiwa na wanafunzi wote 1,592,033 (100%). Kati yao, wanafunzi 72,607 (4.56%) walipata alama zote 14 ambao ni ufaulu mzuri sana, na wanafunzi 286,996 (18.03%) walipata alama 10 hadi 12 ambao ni ufaulu mzuri. Kwa upande mwengine, wanafunzi 353,137 (22.18%) walipata alama 6 hadi 8 ambao ni ufaulu wa wastani, na wanafunzi 879,293 (55.23%) walipata alama 0 hadi 4 ambao ni ufaulu hafifu. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwa kuwa wanafunzi 712,740 (44.77%) tu ndio walipata alama kuanzia 6 hadi 14. Chati Na. 3 inaonesha kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 3.



### **Chati Na 3: Ufaulu wa Wanafunzi katika Swalii la 3**

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi 72,607 (4.56%) waliopata alama zote 14 walikuwa na maarifa ya kutosha kwani walijibu vipengele vyote 7 kwa usahihi. Wanafunzi 286,996 (18.03%) waliopata alama 10 hadi 12 walikuwa katika kiwango kizuri cha ufaulu kwa sababu walijibu kwa usahihi vipengele 5 hadi 6 kati ya 7.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 353,137 (22.18%) waliokuwa na kiwango cha wastani walipata kati ya alama 6 hadi 8 kwa sababu walijibu kwa usahihi vipengele 3 hadi 4 kati ya 7. Hata hivyo, wanafunzi 879,293 (55.23%) waliokuwa na kiwango hafifu cha ufaulu walipata kati ya alama 0 hadi 4. Wanafunzi hao, hawakujibu kipengele chochote au walijibu kwa usahihi kipengele 1 au 2 kati ya vipengele 7.

(i) Rasilimali zina faida gani?

Swali lilimtaka mwanafunzi kubaini faida za rasilimali. Katika kipengele hiki, ufaulu ulikuwa mzuri. Wanafunzi wengi walibaini kwa ufasaha faida za rasilimali kuwa ni *kuingizia wilaya yetu fedha*

*nyingi*. Hii inadhihirisha kuwa, wanafunzi hao walielewa kifungu hicho cha habari.

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi waliandika maliasili husika ambayo hayakuwa majibu sahihi badala ya faida zake. Wanafunzi hao waliandika majibu kama vile; *maliasili, mto, bahari, samaki wakubwa na wachanga, biashara, samaki wa maji baridi na tutakosa samaki siku za baadaye*. Baadhi ya majibu yaliyotolewa ni sentensi zilizonakiliwa kutoka kwenye kifungu cha habari. Sentensi hizi hazikuendana na majibu sahihi. Majibu hayo yalionesha kwamba wanafunzi hao hawakuwa na stadi za kusoma na kuelewa maudhui ya habari kwa kuwa walishindwa kubainisha faida za rasilimali tulizonazo katika jamii.

(ii) Taja faida moja ya uvuvi.

Swali hili lilimtaka mwanafunzi kutaja faida moja tu ya uvuvi. Ufaulu katika kipengele hiki ulikuwa mzuri, kwani baadhi ya wanafunzi walibainisha kwa usahihi kuwa *hutupatia chakula, fedha na ajira*. Wanafunzi hao walitambua faida ya shughuli za uzalishaji mali katika jamii.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi walipata ufaulu hafifu katika kipengele hiki kwani walishindwa kubaini faida za uvuvi. Baadhi yao walitaja aina za uvuvi kama vile; *uvuvi wa maji chumvi, na maji baridi*. Vile vile, wengine waliandika majibu kama vile; *kutumia nyavi, hutegemea eneo na aina ya samaki na kupata samaki wengi* badala ya faida za uvuvi. Majibu hayo yaliashiria kwamba wanafunzi hao hawakuelewa matakwa ya swali, hivyo walinakili baadhi ya maneno au sentensi kutoka katika kifungu cha habari.

(iii) Ni aina gani ya samaki huvuliwa katika mto

Kipengele hiki kilipima uwezo wa mwanafunzi kubaini aina ya samaki anaevuliwa mtoni. Ufaulu katika kipengele hiki ulikuwa wa kiwango kizuri kwani wanafunzi wengi walibaini kuwa *samaki wa maji baridi* ndiyo huvuliwa mtoni. Hii inamaanisha kuwa, wanafunzi hao walibaini kuwa mito huwa na maji baridi hivyo, samaki wanaopatikana humo ni wa maji baridi. Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi waliandika majibu yasiyo sahihi kama vile *samaki wa maji chumvi*, ambao huvuliwa baharini. Wengine walitaja *samaki wakubwa na wachanga*, na wengine walitaja vifaa vinavyotumika katika uvuvi, mfano *wavu nandoano*.

(iv) Ni aina ipi ya uvuvi hufanyika Baharini?

Kipengele hiki kilimtaka mwanafunzi kubaini aina ya uvuvi unaofanyika baharini. Ufaulu katika kipengele hiki ulikuwa wa wastani, kwani baadhi ya wanafunzi walibainisha kwa usahihi kuwa *uvuvi wa maji chumvi* ndio unaofanyika baharini. Jibu hili ni kiashiria kuwa wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kutosha kusoma habari na kubaini ujumbe mahususi uliokuwemo katika habari hiyo.

Hata hivyo, katika kipengele hiki, baadhi ya wanafunzi hawakuandika jibu sahihi, badala yake waliandika namna uvuvi unavyofanyika kama vile; *kuna uvuvi wa kutumia ndoano, uvuvi wa kutumia nyavu na kuvua samaki wakubwa*. Majibu haya yanaonesha kwamba wanafunzi hao hawakuwa na stadi za kusoma na kuelewa maudhui ya habari.

(v) Ni athari ipi husababishwa na uvuvi wa samaki wachanga?

Swali lilimtaka mwanafunzi kubaini athari zinazosababishwa na uvuvi wa samaki wachanga. Ufaulu katika kipengele hiki ulikuwa wa wastani kwani baadhi ya wanafunzi walibainisha kwa usahihi kuwa

husababisha *kukosekana* kwa samaki siku za bade. Hii inadhihirisha kuwa, wanafunzi hao walielewa athari za kuvua samaki wachanga kutoka katika kifungu cha habari.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi walikua na ufaulu hafifu katika kipengele hiki, kwani hawakubaini athari zinazosababishwa na uvuvi wa samaki wachanga. Baadhi ya wanafunzi hao waliandika; *huvua samaki wakubwa na wachanga, kuvua kwa kutumia nyavu zenyenye matundu madogo, na kuvua kwa kutumia ndoano.* Wanafunzi hao hawakubaini athari zinazosababishwa na uvuvi wa samaki wachanga kutoka katika kifungu cha habari walichopewa.

(vi) Ni njia ipi ya uvuvi hutupatia samaki wengi?

Kipengele hiki kilimtaka mwanafunzi kubaini njia ya uvuvi inayotupatia samaki wengi. Ufaulu katika kipengele hiki ulikuwa wa wastani, kwani baadhi ya wanafunzi walibainisha kuwa *uvuvi kwa kutumia wavu* kuwa ndio hutupatia samaki wengi. Jibu hili ni kiashiria kuwa wanafunzi hao walikuwa na stadi nzuri za kusoma na kuelewa habari ipasavyo.

Wanafunzi walioshindwa kipengele hiki waliandika majibu kama vile; *uvuvi unaofanyika baharini.* Wanafunzi hao walihusianisha ukubwa wa bahari na wingi wa samaki, kitu ambacho sio kweli. Wanafunzi hao walipaswa kuelewa kuwa hata baharini wapo wavuvi wanaotumia ndoano ambao huvua samaki wachache kuliko wavuvi wanaotumia nyavu. Kwa hiyo, ilikuwa muhimu kwa wanafunzi kubainisha aina ya vifaa badala ya maeneo ya kuvulia.

(vii) Ipi ni athari ya kuvua samaki kwa kutumia wavu wenye matundu madogo?

Kipengele hiki kilimtaka mwanafunzi kubaini athari ya kuvua samaki kwa kutumia wavu wenye matundu madogo. Ufaulu katika kipengele hiki ulikuwa wa kiwango kizuri. Wanafunzi wengi walibaini athari ya kuvua samaki kwa kutumia wavu wenye matundu madogo kuwa ni *kuvua samaki wachanga*. Wanafunzi hao waliendelea kufafanua kuwa jambo hilo husababisha kukosekana kwa samaki siku za bade. Hii inamaanisha kuwa, wanafunzi hao walisoma na kuelewa kifungu cha habari walichopewa.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi walipata ufaulu hafifu katika kipengele hiki, kwani hawakubaini athari ya kuvua samaki kwa kutumia wavu wenye matundu madogo. Hata hivyo, baadhi yao walijibu kwa kuandika majibu kama vile; *kuvua kwa kutumia ndoano*, kitu ambacho hakiathiri mazalia ya samaki. Wanafunzi wengine katika kundi hili walitoa majibu ya aina ya samaki ambao ni *samaki wa maji baridi* na *samaki wa maji chumvi*, ambayo siyo takwa la kipengele hiki. Aidha, wanafunzi wachache katika kundi hili, walijibu umuhimu wa kuvua samaki, kama vile; *hutupatia chakula, fedha na ajira*. Hii inadhihirisha kuwa wanafunzi hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu shughuli za uzalishaji mali katika jamii. Vielelezo Na. 3.2 na 3.3 vinaonesha mifano wa majibu mazuri na mabaya ya swali la 3.

(i) Rasilimali zina faida gani?

hutupatia fedha zyingi

(ii) Taja faida moja ya uvuvi.

Faida Uvuvi koy hutupatia wakazi ajira na fedha

(iii) Ni aina gani ya samaki huvuliwa katika mto?

Samaki wa maji baridi

(iv) Ni aina ipi ya uvuvi hufanyika Baharini?

Samaki wa maji chumvi

(v) Ni athari ipi ya husababishwa na uvuvi wa samaki wachanga?

Samaki wachanga wakivuliwa eneo hili litakosa  
samaki Siku za baadaye

(vi) Ni njia ipi ya uvuvi hutupatia samaki wengi?

Wavuvi wanaotumia wavu hutupata Samaki  
wengi Zaidi kujikio wale wanotumia ndoano

(vii) Ipi ni athari ya kuvua samaki kwa kutumia wavu wenye matundu madogo?

huvua Samaki wakubwa na wachanga.

### **Kielelezo Na. 3.2: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 3**

(i) Rasilimali zina faida gani?

Rasilimali ni mukurangwe una samathika simu samati, uamogi baldi uvuvi unatanyiha baharini huviwa unuvuila magi

(ii) Taja faida moja ya uvuvi.

UVUVIWA HUTEPYE MTO HUTUWA UNUVIWA MAGI BALDI RAJAMATI UHLE HUTUWA SAMATI UZA MAGI CHUANDI NA SAMATI UATTE HUTUWA SAMATI

(iii) Ni aina gani ya samaki huveliwa katika mto?

eneo na aina za samati hong uvubi uki matumia maliu eno ndooana wauvvi eno ndooana maliu uti kua na matundu madogo huu na Athari

(iv) Ni aina ipi ya uvuvi hufanyika Baharini?

samati uahubua na wachanga samato wachanga ukti ukuuwa eno hilo ukakosa madaki cimreza baadie

(v) Ni athari ipi ya husababishwa na uvuvi wa samaki wachanga?

ambao huingizidai uilava zetu Fenye nyi magi Tim mto na bahari ambayo samati huvuliwa tundu hajira ya dhatu

(vi) Ni njia ipi ya uvuvi hutupatia samaki wengi?

samaki uahubua na wachanga samati unthanga ukti ukuuwa eno hilo uka hosa samaki eimura baadie

(vii) Ipi ni athari ya kuvua samaki kwa kutumia wauwenye matundu madogo?

wauwenye matundu madogo huu na Athari


### Kielelezo Na. 3.3: Sampuli ya majibu Yasiyosahihi katika Swali la 3

Katika kielelezo Na. 3.3 mwanafunzi amenakili maneno yaliyoko katika kifungu cha habari na kuyafanya majibu badala ya kujibu maswali aliopewa.

## **2.2.2 Swali la 4: Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya kila Siku.**

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kutumia Ramani na Elimu ya Anga Katika Maisha ya Kila Siku*. Swali lililenga kupima umahiri mahususi wa *Kutumia Ramani Katika Mazingira Yanayomzunguka*. Katika swali hilo, wanafunzi walitakiwa kutaja vipengele vinne muhimu vya kuzingatia wakati wa kuchora ramani ya shule yao.

Swali hili lilijibowi na wanafunzi wote 1,592,033 (100%). Kati yao, wanafunzi 191,169 (12.01%) walipata alama zote 8 ambaao ni ufaulu mzuri sana, na wanafunzi 121,592 (7.64%) walipata alama 6 ambaao ni ufaulu mzuri. Kwa upande mwengine, wanafunzi 105,212 (6.61%) walipata alama 4 ambaao ni ufaulu wa wastani, na wanafunzi 1,174,060 (73.75%) walipata alama 0 hadi 2, ambaao ni ufaulu hafifu. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu kwani ni wanafunzi 417,973 (26.26%) tu walipata kati ya alama 4 hadi 8. Chati Na. 4. inaonesha kiwango cha ufaulu katika swali la 4.



**Chati Na.4:** Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 4

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, wanafunzi 191,169 (12.01%) waliopata alama 8 walikuwa na uelewa wa juu wa kutambua matumizi ya ramani katika mazingira. Wanafunzi hao walibainisha kwa usahihi vipengele vinne muhimu vya kuzingatia wakati wa uchoraji wa ramani. Kwa ujumla, kuna vipengele vitano, lakini katika swali hilo, wanafunzi walitakiwa kubainisha vipengele vinne kati yake. Vipengele hivyo vilikuwa; *Mpaka au Fremu ya ramani, Ufunguo, Kichwa cha ramani, Dira na Kipimio cha ramani.* Hii inadhihirisha kuwa, wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa matumizi ya ramani. Kielelezo namba 4.1 ni sampuli ya majibu sahihi katika swali hili.

4. Wanafunzi wa Darasa la Nne walitakiwa kuchora ramani ya shule yao. Ni vipengele vipi vya ramani wanapaswa kuzingatia wakati wa kuchora ramani? Bainisha vipengele vinne.

- (i) *Dira*.
- (ii) *Ufunguo*.
- (iii) *fikra cha ramani*.
- (iv) *Mipaka*.

**Kielelezo Na: 4.1: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 4**

Vilevile, wanafunzi 121,592 (7.64%) waliopata alama 6 katika swali hili walibainisha kwa usahihi vipengele vitatu kati ya vinne vilivyotakiwa. Aidha, wanafunzi hao walitaja kipengele kimoja kisicho sahihi, au hawakuandika kipengele cha nne, hivyo kupata alama pungufu. Hii ilidhihirisha kuwa wanafunzi hao walikuwa na uelewa kuhusu vipengele muhimu vinavyohitajika katika uchoraji wa ramani, lakini hawakukumbuka kipengele kimojawapo.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 214,359 (13.46%) waliopata kuanzia alama 2 hadi 4, walikuwa na uelewa wa wastani wa vipengele muhimu vya kuzingatia katika uchoraji wa ramani. Baadhi yao walibainisha kwa kuchanganya vipengele muhimu viwili sahihi, na viwili visivyo sahihi. Vilevile, kulikuwa na wanafunzi wachache waliobainisha kipengele kimoja sahihi, na vitatu visivyo sahihi. Zaidi ya hapo, wanafunzi wengine katika kundi hili walibainisha kipengele kimoja sahihi, lakini ikiwa na tahjia iliyokosewa.

Hata hivyo, wanafunzi wengi 1,064,913 (66.89%) waliopata 0 hawakutambua vipengele muhimu vya kuzingatia wakati wa uchoraji

wa ramani. Baadhi yao hawakuelewa matakwa ya swali. Badala ya kutaja vipengele hivyo, walitaja umuhimu wa ramani kama vile; *husaidia wasafiri kujua mwelekeo*, *husaidia kujua mipaka ya eneo*, *husaidia katika ujenzi wa miundo mbinu na husaidia kufahamu sura ya nchi*. Wanafunzi wengine katika kundi hili, waliandika aina za ramani, kwa mfano; *ramani ya takwimu*, *ramani ya topografia na ramani ya picha*. Wanafunzi wachache katika kundi hili walipotoka kwenye matakwa ya swali, na kutaja vitu vinavyopatikana katika mazingira ya shule, kama vile; *mawe yaliyopangwa au matofali*, *maua, madarasa, ofisi ya walimu, viwanja vya mpira na madawati*. Huu ni uthibitisho kuwa, wanafunzi hao hawakuelewa vizuri matumizi ya ramani katika mazingira. Kielelezo 4.2 kinaonesha majibu ya mwanafunzi yasiyo sahihi katika swali hilo.

4. Wanafunzi wa Darasa la Nne walitakiwa kuchora ramani ya shule yao. Ni vipengele VIPI VYA RAMANI WANAPASWA KUZINGATIA WAKATI WA KUCHORA RAMANI? Bainisha vipengele vinne.

- (i) Madarasa.
- (ii) Vyoo Vya walimu.
- (iii) Nyumba za walimu.
- (iv) Vyoo Vya wanafunzi.

**Kielelezo Na: 4.2. Sampuli ya Majibu yasiyo Sahihi katika Swali la 4**

Katika kielelezo Na. 4.2, mwanafunzi aliorodhesha majengo yanayopatikana katika maeneo ya shule ambayo ni madarasa, vyoo vya walimu, nyumba za walimu na vyoo vya wanafunzi kinyume na matakwa ya swali. Alitakiwa kuorodhesha vipengele vinne vinavyotakiwa kuzingatiwa wakati wa kuchora ramani ambavyo ni

kati ya Mipaka au Fremu, Ufunguo, Kichwa cha ramani, Dira na Kipimio cha ramani.

### **3.0 TATHIMINI YA UFAULU KWA KILA UMAHIRI**

Uchambuzi katika Upimaji wa Darasa la Nne (SFNA) 2022 unaonesha kuwa, kati ya umahiri mkuu wa aina nne uliopimwa (kama ulivyoainishwa kwenye muhtasari wa Elimu ya Msingi wa somo la Maarifa ya Jamii wa mwaka 2016), kiwango cha ufaulu kilikuwa kizuri katika umahiri wa aina mbili. Kiwango cha ufaulu kilikuwa cha wastani katika umahiri mmoja, na hafifu katika umahiri mwingine. Umahiri uliofanya vizuri zaidi ni *Kutambua Matukio Yanayotokea katika Mazingira Yanayomzunguka* ambao ulikuwa na ufaulu wa asilimia 74.34. Umahiri wa *Kutambua Misingi ya Uzalendo katika Jamii* ulikuwa na ufaulu mzuri wa asilimia 72.46. Kwa upande mwingine, kiwango cha ufaulu katika umahiri wa *Kufuata Kanuni za Kiuchumi katika Shughuli za Uzalishaji Mali* ulikuwa ni wa wastani kwa asilimia 44.77. Umahiri wa *Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya Kila Siku* ulikuwa na ufaulu hafifu kwa asilimia 26.25. Ijapokuwa wanafunzi wengi wameweza kupata umahiri unaokubalika katika mahiri tatu, bado wanafunzi hao wana upungufu wa umahiri unaotarajiwa. Muhtasari wa ufaulu katika kila umahiri umeoneshwa katika **Kiambatisho**.

### **4.0 HITIMISHO**

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika maswali ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne 2022 katika somo la Maarifa ya Jamii umeonesha kiwango kizuri katika umahiri wa *Kutambua Matukio Yanayotokea Katika Mazingira Yanayomzunguka* na *Kutambua Misingi ya Uzalendo Katika Jamii*. Uchambuzi zaidi umeonesha kiwango cha wastani katika umahiri wa *Kufuata Kanuni za Kiuchumi*

*Katika Shughuli za Uzalishaji Mali na hafifu katika umahiri wa Kutumia Ramani na Elimu ya Anga Katika Maisha ya Kila Siku.* Aidha, kuna changamoto zilizosababisha baadhi ya wanafunzi wasifanye vizuri. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na kushindwa kuelewa hitaji la maswali, ujuzi hafifu katika umahiri mahususi na kushindwa kuhawilisha maarifa na ujuzi kutoka katika jamii inayowazunguka. Vilevile, baadhi ya wanafunzi walionesha uwezo mdogo wa kujua kusoma na kuandika. Hali hii imejidhihirisha katika ufaulu wa swali la 3 linalohitaji stadi za kutosha za kusoma kwa uelewa na kuandika.

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi waliweza kuonesha umahiri wa kutosha uliowawezesha kubaini majibu sahihi katika maswali yaliyoulizwa na hivyo kuwa na ufaulu mzuri.

## **5.0 MAPENDEKEZO**

Ili kuboresha kiwango cha utendaji wa wanafunzi, Baraza la Mitihani la Tanzania linapendekeza mambo yafuatayo:

- (a) Walimu wasisitizwe kupima umahiri wa wanafunzi katika stadi za kusoma na kuandika ili kuweza kuwasaidia wanafunzi walio na ujuzi mdogo wa kusoma na kuandika. Hii itawafanya waweze kutambua matakwa ya swali na kueleza hoja zao kwa ufasaha.
- (b) Baadhi ya wanafunzi walionesha udhaifu katika ujuzi wa ufahamu. Mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji zitumike katika masomo yanayolenga kukuza ujuzi wa ufahamu wa wanafunzi. Kwa mfano, wanafunzi wapewe matini ya kusoma na kuelezea ujumbe uliomo katika matini husika.
- (c) Walimu wasisitizwe kuwaongoza wanafunzi katika matumizi ya vitendo halisi katika ufundishaji na ujifunzaji. Hii ni pamoja na kufanya ziara za kimasomo maeneo mbalimbali

yanayoweza kuwajengea wanafunzi uwezo wa kupata umahiri mahususi.

- (d) Wanafunzi wapewe mazoezi ya kutosha yanayolenga kukuza umahiri ili kuwajengea uwezo katika kujibu maswali yanayopima umahiri. Kwa mfano, wanafunzi wapewe mazoezi mengi ya kuchora ramani kwa kuzingatia vipengele vya lazima vya ramani. Aidha, wanafunzi wafanye mazoezi ya kueleza hatua za kufuata wanapochora ramani.

## KIAMBATISHO

### 03 Maarifa ya Jamii - Ulinganifu wa Ufaulu kwa Wanafunzi katika kila Umahiri kwa Mwaka 2021 na 2022

Na.	Umahiri	SFNA 2021				SFNA 2022			
		Ufaulu wa kila Swalii		Wastani wa Ufaulu (%)	Maoni	Ufaulu wa kila Swalii		Wastani wa Ufaulu (%)	Maoni
		Namba ya Swalii	% ya Ufaulu			Namba ya Swalii	% ya a Ufaulu		
1	Kutambua Matukio Yanayotokea Katika Mazingira Yanayomzungu ka	1	82.80	82.80	Mzuri	2	74.34	74.34	Mzuri
3	Kutambua Misingi ya Uzalendo Katika Jamii	3	28.50	28.50	Hafifu	1	72.46	72.46	Mzuri
	Kufuata Kanuni za Kiuchumi Katika Shughuli za Uzalishaji Mali	2	70.70	70.70	Mzuri	3	44.77	44.77	Wastani
4	Kutumia Ramani na Elimu ya Anga Katika Maisha ya Kila Siku	4	39.70	39.70	Wastani	4	26.25	26.25	Hafifu

